*S.1 KISWAHILI

KUTAMKA SAUTI ZA

LUGHA YA KISWAHILI** .

Shughuli 1.1 Kusikiliza na Kuzungumza

Katika vikundi,

Tamka, kariri, na kusoma kwa sauti maneno yafuatayo kwa kuzingatia matamshi bora ya vokali za Kiswahili.

a- anza, baba, kaka, dada

e- endesha, endelea,

i.inuka, ingia, bibi, mimi, sisi

o- omba, ona, ondoa, oga, wote

u- uhuru, umoja, kuku, nguvu

2. Tamka maneno yafuatayo yenye matumizi ya vokali mbili

aa- kaa, jaa, baada, saa,

ee- mzee, pekee

ii- tii, bidii

oo- choo, njoo

uu- juu, mguu

3. Tamka maneno yafuatayo yenye matumizi ya vokali mbili zisizofanana

ondoa, lia, ongea, fagia, pokea, chuo, kimbia, somea

4. Shirikiana na wenzako kutambua, kutamka na kuandika baadhi ya maneno yenye vokali mbalimbali.

3

Shughuli 2.1 Kusikiliza na Kuzungumza

Katika vikundi,

1. Tamka sauti zifuatazo.

i. /b/, /p/, /m/ /w/

ii. /f/, /v/

iii. /dh/, /th/

iv. /d/, /l/, /n/, /r/, /s/, /t/, /z/

v. /ch/, /j/, /ny/, /sh/, /y/

vi. /k/, /g/, /ng'/, /gh/, /kh/

vii. /h/.

2. Tamka tena sauti zilizo juu. Tambua mahali sauti hizo zinakotamkiwa.

3. Unganisha konsonanti na vokali ulizotamka hapo juu kuunda silabi na maneno.

4. Shirikiana na wenzako katika kikundi kuandika alfabeti ya Kiswahili kutoka A hadi Z.

Funzo b. Kutambua msamiati wa watu wa nyumbani

Shughuli 3.1 Kusikiliza na kuzungumza

Katika vikundi,

1. Taja watu unaoishi nao nyumbani

2. Jadiliana na wenzako kutafuta maana ya maneno uliyopewa katika boksi

baba, mama, kaka, dada, bin, binti, shangazi, babu, nyanya

3. Elezea kuhusu watu wa familia yako kwa kutaja majina yao.

4. Shirikiana na wenzako kusoma na kujadili maana ya sentensi zifuatazo

i. Baba yangu ni dereva wa basi.

ii. Mama yangu ni mwalimu wa Kiswahili.

iii. Dada yake Peter anafundisha katika Chuo Kikuu cha Kyambogo.

iv. Bin yangu anaitwa Haba.